# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz
SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA WIZARA YA AFYA**

**Mheshimiwa Spika,**
Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu tayari kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Uongozi mzima wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawataka wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *9.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, Kanuni ya *108(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Hivyo, baada ya utangulizi huo sasa naomba kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Wizara ya Afya ambapo jumla ya mapendekezo 53 tuliyaliwasilishwa kwa Wizara na yote tunashukuru yameweza kuyapatia majibu ya kina.

## HOSPITALI YA MNAZIMMOJA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inapenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa juhudi kubwa alizozichukua katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi hususan kwa Wizara ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,**
Licha ya uboreshaji wa maslahi hayo ya wafanyakazi wa kada za afya, Kamati imebaini bado kuna changamoto katika ongezeko hilo lililoongezwa halikuzingatia Muundo wa Utumishi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja uliopendekezwa hususan Kada za Madaktari Bingwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati imegundua kutokana na ongezeko hilo la maslahi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya limepelekea kuondolewa kwa Posho la Mazingira Magumu kwa wafanyakazi hao, hivyo kupelekea watendaji hao kujiona wameachwa mkono.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na mapungufu hayo, Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuliangalia upya suala la upandishaji wa mishahara kwa kuzingatia Miundo ya Utumishi ya Wizara husika pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika Kilele cha Sherehe ya Siku ya Wafanyakazi.

## WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kamati haikufurahishwa na utekelezaji wa Mapendekezo waliyoyatoa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2021/2022 katika suala zima la ujazaji wa nafasi tano zilizowazi za uongozi pamoja na Bodi ya Wakala huo kufanya kazi kwa muda wa miaka mitano na Mwenyekiti tu bila ya kuwepo kwa Wajumbe, hali iliyopelekea Wakala huo kushindwa kutekeleza majukumu yao na kufikia maamuzi juu ya masuala yanayohusiana na utendaji wa Wakala huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kuharakisha upatikanaji wa Wajumbe hao wa Bodi ya Wakala, ili kuweza kuondoa changamoto utekelezaji wa majukumu yao kama yanavyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria katika kujaza nafasi za wakurugenzi.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kuandaa Mpango Madhubuti wa ufuatiliaji wa deni la Wakala wanalodai Jeshi la Polisi licha ya mazungumzo pamoja na juhudi kubwa zilizochukuliwa na Wakala huo, bado juhudi hizo hazijazaa matunda na mpaka kufikia Juni, 2022 Jeshi hilo linadaiwa shilingi Milioni Mia Mbili na Moja, Laki Mbili na Sabiini na Saba (201,277,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na ucheleweshwaji huo wa ulipaji wa deni, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kulitafutia ufumbuzi suala hilo, ili kusaidia kupunguza malalamiko ya muda mrefu kwa kazi wanazozipeleka Jeshi hilo kwa Wakala kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara.

## UONGOZI NA UTAWALA WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa kipekee, Kamati inachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Marais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kujenga Hospitali za Wilaya na Mikoa kwa Unguja na Pemba kupitia fedha za Ahuweni za UVIKO 19. Kamati, ina matumaini makubwa kwamba majengo hayo ya kisasa yatakuwa na vifaa vya kisasa na kuweza kutoa huduma za afya zilizobora na salama kwa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Uwepo wa majengo hayo utakwenda sambamba na wafanyakazi wenye ujuzi, weledi na taaluma zinazohitajika katika hospitali zetu hizo mpya. Hivyo, Kamati inatoa wito kwa wafanyakazi kufanya kazi kwa uzalendo kwa nchi yao, ili kuweza kufikia azma na malengo yaliyokusudiwa ya kujengwa kwa hospitali hizo. Aidha, kutimiza malengo ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 kwamba Matibabu Bure kwa wananchi wote.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya maelezo hayo machache, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………………….,
Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**